Kumekuwepo na changamoto kubwa ya lugha ya Kiingereza kwa baadhi ya wanafunzi wanaoshiriki maonyesho hayo, kwani wengi wanatoka katika shule tofauti tofauti.

Wale wanaojieleza vizuri kwa lugha hiyo ni wanaotoka kwenye shule za binafsi (maarufu kama English Medium) na wanaweza kueleza vyema hata kama wazo lao litakuwa la kawaida tu.

Lakini walio wengi ambao wanatoka katika shule za umma, licha ya kuwa na mawazo mazuri, hushindwa kujieleza vyema kwa Kiingereza, jambo ambalo kwa namna moja ama nyingine linaweza kuwa kikwazo.

Ni vyema basi serikali ikaandaa mitaala ambayo itatoa fursa ya Kiswahili kutumika katika ufundishaji, kwa sababu ubunifu mara nyingi hauhitaji tu kuongea, wakati mwingine ni vipaji vya watu.

**Sunday, July 29, 2018**

**JIJILETU BLOG**

**MAONYESHO YA WANASAYANSI CHIPUKIZI KUANZA AGOSTI 1 MWAKA HUU**

Na Humphrey Shao, Globu ya Jamii

Tasisi ya Young Scientist inataraji kuanza Maonyesho yake ya Wanasayansi Chipukizi kuanzia Agosti 1 mpaka 2 mwaka huu.

Akizungumza wakati wa mkutano wake na waandishi wa Habari Mwanzilishi wa YST Nchini,Dr Gosbert Kamugisha amesema kuwa Maonyesho hayo ambayo yanataraji kufanyika katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam na kushirikisha sekondari 100 nchini.

“kwa siku mbili maonyesho ya wanasayansi Chipukizi wataonyesha kazi zao katika Nyanja mbalimbali za Sayansi kama kemia ,fizikia na hesabu ,biologia na Mazingira , sayansi ya jamii na ugunduzi wa wanasayansi chipukizi” amesema Dr Kamugisha.

Ametaja kuwa wanasayansi chipukizi wataonyesha ugunduzi mzuri Zaidi watazawadiwa pesa taslimu na wanasayansi wanne watapata ufadhili wa masomo ya chuo kikuu ambao utatolewa na shirika la Karimjee foundation ili waweze kuendelea kuimarisha vipaji vyao.

Maonyesho ya wanasayansi chipukizi 2018 yanalenga kuwahamasisha wanafunzi wa Sekondari kupenda Sayansi na ugunduzi na kujenga utamaduni wa kisayansi kwa vijana wa Tanzania.



Mwanzilishi wa tasisi ya Young Scientist nchini, Dr Gosbert Kamugisha akizungumza na Waandishi wa Habari juu ya Maonyesho ya Nane ya Wanasayansi Chipukizi.



Mwanzilishi Mwenza wa Tasisi ya Young Scientist Tanzania kutoka nchini Ireland akizungumza na Waandishi wa Habari juu ya Maonyesho ya Wanasayansi Chipukizi



Patricia Mhondo Meneja mahusiano kutoka kampuni ya Shell Tanzania akizungumza juu ya kampuni hiyo kudhamini maonyesho hayo.



Devota Rubama Meneja wa Mahusiano wa Karimjee Foundation





## MEDIA COVERAGE DURING YOUNG SCIENTISTS EXHIBITION

### TELEVISIONS

a) **ITV**

The story was aired at 2000pm

**News summary**; the government has been impressed by students ability to develop special gadget for protecting people with albinism, and declare to develop special schools. Minister said during the YST exhibition held in Dar es Salaam.

**View at :**

https://www.dropbox.com/s/u67rbtecy8epu1v/TV%20-%20ITV.mp4?dl=0

b) **Azam TV**

The news was aired at 2000pm evening

**News summary**: Msalato Girl's Secondary School students emerged winners of the YST 2018

c) **EATV**

The story was aired at 2000pm evening

**News summary**: Kibiti secondary students come up with technology to protect people with albinism when they face with trouble. While minister Ndalichako vow to develop students' talents.

View at :

https://www.dropbox.com/s/gt4qolyzjewwpf1/TV%20-%20EATV.mp4?dl=0

d) **Channel Ten**

The story was aired at 1900pm

**News summary**: The government has urged the Commission for Science and Technology (Costech) to supervise and develop science talents ofprimary and secondary students in order to encourage students to study science subjects.

**View at:**

https://www.dropbox.com/s/i1a9hkl5t4nkxpq/TV%20-%20CHANNEL%2010.mp4?dl=0

**RADIOS**;

a) **Upendo fm radio**

The story was aired at 1900pm

**News summary**: the government has encouraged the society to help young scientists achieve their dreams through science.

**Listen at:**

https://www.dropbox.com/s/kgof7qri5ghra3a/RADIO%20-%20UPENDO%20FM.mpeg?dl=0

b) **Efm radio**

The story was aired at1900pm

***News summary***: Young scientists develop a technology to help people with albinism to protect them from abduction.

c) **East Africa radio**

The story was aired at 1900pm

***News summary***; the government has been impressed by the technology developed by students to use hair to produce manure during the YST exhibition.

**Others:**

**ZBC Radio**

**https://www.dropbox.com/s/fkswyjz9ej1re3h/RADIO%20-%20ZBC%20RADIO.mp4?dl=0**

**NEWSPAPERS**

The Guardian

The story was published on August 4, 2018

***News summary***; Ndalichako reaffirms efforts to girls' science, technology embrace

# Ndalichako reaffirms efforts to girls' science, technology embrace

**By Correspondent James Kandoya**

THE government has reaffirmed its commitment to continue engaging other stakeholders in efforts aimed to help young people especially girls, embrace and channel technology for betterment of their life opportunities.

The Minister for Education, Science and Technology, Prof. Joyce Ndalichako affirmed this position at the formal launching of the 8th Annual Scientific Exhibition in Dar es Salaam yesterday, attended by over 200 students from the Mainland and Zanzibar.

Experience had shown that there was no developed nation that hadn't hugely invested in science, she said, noting that investing in youths was crucial for development to be assured in the next generation.

The minister noted Young Scientist Tanzania (YST) collaboration with various partners resonates with the fifth phase government agenda of reaching an industrial economy.

"I would like to assure you that the government will continue working with partners to inculcate a culture of pursuing science subjects in order to realize an industrial economy by 2025," she said.

Prof. Ndalichako urged YST to forge collaboration with higher learning institutions in the country to ensure that young people, and especially women, embrace and channel technology for wide ranging purposes.

"So much positive change can come from harnessing innovation and technology through the imagination of youth - it can open their minds, show them the power of what they can achieve to work toward a positive future," the minister underlined.

YST Executive Director Dr Gosbert Kamugisha said that during this year's exhibition more than 200 applications had been received so far.

"YST is proud of the works submitted from different applicants from the Mainland and Zanzibar. What they need is your support," he said.

"Technology and science have the power to transform lives - to take humankind where no one has gone before, effect change, and better the Earth and beyond.

"But the current cohort of young people, so far the most technologically integrated generation, has the potential to use technology for what is good."

Representing the Karimjee Jivanjee Foundation (KJF), Jasmine Karimjee said "our duty is to create a platform for young scientists to show case their work."

Karimjee Jivanjee provide university scholarships to overall winners in each year's scientific exhibition, where it has up to now injected over 25 million dollars for the purpose.

During the exhibition, Msalato Girls secondary school of Dodoma emerged the overall winner followed by St Juhudi Secondary school of Arusha as runners up.

**The Guardian**; Photo was published on August 4, 2018

Caption; Education, Science, Technology and vocational training minister Prof. Joyce Ndalichako (R) presents a trophy to Msalato Girls Secondary School students Farida Kwingwa (2nd R) and Wilhemina Martin Msemwa after they emerged first winners in a Young Scientists exhibition held in Dar es Salaam on Thursday. Others are Marc den Hartog (L) and Jasmine Karimjee.



Education, Science, Technology and Vocational Training Minister Prof. Joyce Ndalichako (R) presents a trophy to Msalato Girls Secondary School students Farida Kwingwa (2nd R) and Wilhelimina Martin Msoma after they emerged first winners in a Young Scientists exhibition held in Dar es Salaam on Thursday. Others are Marc den Hartog (L) and Jasmeen Karimjee. PHOTO: Correspondent Getrude Mpezya

Daily News
The story was published on August
***New summary***; 2 Msalato schoolgirls scoop YST award



# 2 Msalato schoolgirls scoop YST award

By CHRISTINA MSEJA

TWO students of Msalato Girls Secondary School in Dodoma Region emerged winners of the Eighth Young Scientists Tanzania (YST) exhibition and competition for designing an Exploration of salt Content in Herbs 'vibigili' for animal feed.

At the event held in Dar es Salaam, yesterday evening, the Form Four girls Farida [illegible] and Wilhelmina [illegible] were awarded a shield, 1.5 million/- cash and were also offered scholarship by the Karimjee Jivanjee Foundation to study science courses at university.

"Congratulations to the winners of the competition. The government is looking for the best way to support young scientists and their creativities for the development of the country," said the Minister for Education, Science, Technology and Vocational Training, Professor Joyce Ndalichako, who was the guest of honour at the event.

Minister Ndalichako also congratulated YST, who are the organisers of the event and sponsored by BG Tanzania, a subsidiary of Royal Dutch Shell Plc. She commended teachers for their support in training the students and urged the students to work hard to take their innovations further.

"We will continue to improve teaching and learning environment for the better future of our young scientists to develop their talents and skills for the benefit of our country and be able to solve different problems which are found in the society," she said.

She also noted that Tanzania Commission for Science and Technology (COSTECH) should use these young scientists so that in the coming years, Tanzania can get some unique innovations which will be found and made in the country, and surprise the world.

She further called upon all students to come forward and showcase their talents and skills on science studies and become innovators in future.

At the same occasion, the YST Board Chairman, Dr Yunus Mgaya said that the government has provided good support to the innovation sector. The programme has become a national science competition and the students are travelling from all regions across the country to showcase their scientific skills.

"The project is helping students to engage in various [illegible]

**Habari Leo**

The story was published on August 4, 2018

***News summary***; Msalato girls students emerged the overall winner for the YST 2018



HABARI 5

# Msalato wapata tuzo ya wanasayansi chipukizi

Na Lucy Lyatuu

WANAFUNZI wa kidato cha nne kutoka shule ya Sekondari ya Wasichana ya Msalato iliyoko mkoani Dodoma wameibuka washindi katika shindano la wanasayansi chipukizi baada ya kuandika wazo la mradi wa kuutumia mmea wa mbigiri kama moja ya njia ya kutengeneza vyakula vya mifugo kutokana na kuwa na chumvi nyingi.

Aidha serikali imeiagiza Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech) kuangalia mawazo ya miradi iliyoandikwa na wanafunzi hao na kuiendeleza ili kuendeleza kuinua vipaji vya wanafunzi pamoja na kupata wagunduzi.

Waziri wa Elimu, Sayansi,Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi Profesa ,Joyce Ndalichako ndiye alitoa zawadi kwa washindi katika hafla ya shindano la wanasayansi chipukizi iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam.



Wanafunzi Wilhelmia Msoma (kushoto) na Farida Mnyazi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato, wakipokea tuzo kutoka kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknilojia, Profesa Joyce Ndalichako baada ya kutangazwa washindi wakati wa Mkutano Mkuu wa Nane wa Mwaka wa Maonesho ya Sayansi na Teknolojia kwa Wanasayansi Vijana Tanzania (YST) katika hafla ya iliyofanyika Dar es Salaam. (Picha na Venance Nestory).

kwa hali na mali hadi kuufanikisha ukiwa na majawabu chanya wanayosema, ni suluhisho katika mchango wa kuifanya Tanzania ya viwanda kwani mmea huo ukitumika vema, utakuwa malighafi za viwanda na utachochea ufugaji bora kupitia lishe ya mifugo.

Wanasema walimu walijitahidi kuhakikisha mmea huo unapatikana shuleni, kuwasimamia kwa usaidizi unaohitajika hapa na pale na hata kuwasaidia kutayarisha machapisho ya ripoti ya mradi huo.

Kuhusu changamoto, wanafunzi hao wanasema kubwa ilikuwa namna ya kugawa muda wao bila kuathiri ratiba nyingine, hasa muda wa masomo ya darasani.

Wanasema namna ya kukabili changamoto hiyo, ilikuwa ni hasa kutumia muda wao wa ziada na kwamba, changamoto nyingine waliyoiona japo haikutosha kuwakatisha tamaa, ni kuchomwa miiba iliyopo katika mmea huo.

Wanafunzi wanapongeza uwepo wa maabara nzuri shuleni hapo kwani kila kemikali waliyohitaji ili kutambua aina ya chumvi iliyopo katika mmea huo waliipata.

**Mwananchi**

**News summary**; liboru students has develop a system to track mobile communication at school area



# Wanafunzi Ilboru wabuni mtambo kunasa mawasiliano ya simu shuleni

**02**

Idadi ya wanafunzi waliobuni mtambo wa kunasa mawasiliano ya simu kwa wanafunzi wenzao

**Mtambo huo umeunganishwa na 'simu janja' ya mkuu wa shule na msimamizi wa wanafunzi**

Elizabeth Edward, Mwananchi
eedward@mwananchi.co.tz

**Dar es Saaam.** Wanafunzi wawili wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Ilboru iliyopo mkoani Arusha wamebuni mtambao wa kunasa mawasiliano ya simu yanayofanyika ndani ya mazingira ya shule.

Wanafunzi hao, Boris Massesa na Adam Rueben wametengeneza mtambo huo ili kukabiliana na changamoto ya matumizi ya simu kinyemela kwa wanafunzi.

Mtambo huo umewawezesha wanafunzi hao kupata tuzo ya wanasayansi chipukizi katika kipengele cha teknolojia.

Akizungumza na mwandishi wa gazeti la Mwananchi katika hafla ya utoaji wa tuzo hizo iliyoandaliwa na Taasisi ya Young Scientist Tanzania (YST) jijini hapa, Massesa alisema wazo la kutengeneza mtambo huo walilipata mwaka jana baada ya wanafunzi wa kidato cha nne kunaswa wakitumia simu kuvujisha mtihani wa Taifa.

"Jambo hilo lilituuma, tukaumiza kichwa mimi na rafiki yangu ndipo tukapata wazo la kutengeneza mtambo huu," alisema Massesa.

Pia, alisema mtambo huo waliuotengeneza umeunganishwa na 'simu janja' ya mkuu wa shule, msimamizi wa wanafunzi na mwalimu wa nidhamu.

"Endapo mawasiliano yoyote ya simu ya mwanafunzi yatafanyika bwenini au katika mazingira ya ndani ya shule, iwe imepigwa au meseji, kule kwa walimu watapata taarifa."

Aliongeza kuwa tangu mtambo huo umeanza kufanya kazi wanafunzi wanne wamekamatwa.

Waziri wa Elimu, Profesa Joyce Ndalichako alisema: "Sheria haziruhusu mwanafunzi kuwa na simu, lakini wengi wamekuwa wakitafuta namna ya kuwa nazo na kufanya mawasiliano ambayo hayana tija katika masomo yao. Na ndiyo sababu tunapata matokeo mabaya na mabweni kuungua moto, hii yote ni kwa sababu wanafunzi wanahangaika kuchaji simu."

Mwenyekiti wa bodi ya YST, Profesa Yunus Mgaya alisema lengo la wanafunzi kubuni miradi ya kisayansi ni kuleta mabadiliko au kutatua changamoto zilizopo ndani ya jamii.

Katika tuzo hizo wanafunzi wa Shule ya Sekondari Msalato, Farida Mnyazi na Whelmina Msoma waliibuka washindi wa jumla na kuzawadiwa Sh1.3 milioni, udhamini wa masomo ya chuo kikuu kutoka Taasisi ya Karimjee Jivanjee na safari ya Afrika Kusini kutoka Kampuni ya Siemens.

Wanafunzi hao walifanya utafiti na kubaini kiwango cha chumvi kilichopo kwenye mmea aina ya mbigiri kinasaidia afya ya wanyama wanaokula majani.

**Feature article;**

***News summary***; Iliboru students have develop a system to track mobile communication in the school



# Wanafunzi Ilboru watengeneza kifaa kuwanasa wanaotumia simu shuleni



Elizabeth Edward, Mwananchi
eedward@mwananchi.co.tz

Kuendelea kuona changamoto ni kikwazo ni sababu inayowakwamisha watu wengi na kukata tamaa kusonga mbele. Lakini changamoto ikionekana kuwa ni fursa, huo huwa mwanzo mzuri wa maendeleo na kuikwamua jamii kutoka kwenye tatizo sugu.

Hivyo ndivyo walivyofanya Boris Massesa na Adam Rueben kwa kubuni teknolojia inayoweza kunasa mawasiliano ya simu katika eneo ambalo haliruhusiwi simu kutumika.

Wanafunzi hawa wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Ilboru mkoani Arusha wamebuni mtambao unaoweza kunasa mawasiliano ya simu ya wanafunzi yanayofanyika ndani ya mazingira ya shule.

Kwa wanafunzi wa shule za bweni watakuwa wanafahamu hili kuwa licha ya sheria za shule nyingi kukataza wanafunzi kutumia simu wakiwa shuleni, wapo ambao wanatumia simu hizo kwa kificho na kuzificha katika mazingira ambayo ni nadra kwa mwalimu kushtukia.

Lakini wanafunzi hawa ambao si vibaya kuwaita wanasayansi chipukizi, wamekuja na tiba ya uvunjaji huo wa sheria za shule kwa nia njema ya kuwafanya wanafunzi wazingatie zaidi masomo wanapokuwa shuleni.

INAENDELEA UK 22

# watengeneza kifaa kuwanasa wanaotumia simu wakiwa shuleni

INATOKA UK 21

Kipaji cha vijana hawa kimeonekana kwenye maonyesho ya wanasayansi chipukizi yaliyoandaliwa na taasisi ya Young Scientists Tanzania (YST) na kufanikiwa kutwaa tuzo katika kipengele cha teknolojia.

Nyuso zao zikiwa zimegubikwa na furaha vijana hawa wanazungumza na mwandishi wa makala hii na kumueleza kilichowasukuma kutengeneza mtambo huo.

Massesa anasema wazo la kutengeneza mtambo huo liliwajia mwaka jana baada ya kukithiri kwa matumizi ya simu kwa wanafunzi kinyume na sheria za shule zinavyoelekeza.

Anasema, "Ni jambo ambalo lilikuwa linatupa shida na kutuumiza vichwa mimi na rafiki yangu ndipo tulipofikia wazo la kutengeneza kitu ambacho kitatambua endapo mawasiliano yatakuwa yanafanyika miongoni mwa wanafunzi ndani ya shule.

"Hapo tukamfuata mwalimu wa miradi pale shuleni tukamuelezea wazo letu naye akawa pamoja na sisi kwa kuwa lengo letu lilikuwa jema ikizingatiwa kuwa matumizi ya simu ni suala ambalo walimu wamekuwa wakilipigia kelele kwa muda mrefu," anasema Massesa.

Iliwachukua takribani miezi 10 kwa wanafunzi hao kukamilisha mtambo huo ambao tayari umeanza kufanya kazi, huku vifaa vingi wakivinunua kutokana na fedha zao wanazopewa kwa ajili ya matumizi shuleni.

Takribani Sh600,000 wamezitumia kununua baadhi ya vifaa na hatimaye mtambo huo ukakamilika na kuanza kufanya kazi.

**NUKUU**

**"Sheria haziruhusu mwanafunzi kuwa na simu lakini wengi wao wamekuwa wakitafuta namna ya kuwa nazo na kufanya mawasiliano ambayo kwa hakika hayana tija katika masomo yao na ndio sababu tunapata matokeo mabaya na mabweni kuungua moto, hii yote ni kwa sababu wanafunzi wanahangaika kuchaji simu."**

**Profesa Ndalichako.**

## Unafanyaje kazi?

Mtambo huu umeunganishwa na simu za baadhi ya walimu ambao hupelekewa taarifa endapo mawasiliano yoyote yatafanyika bwenini au katika mazingira ambayo mara nyingi wanakuwepo wanafunzi.

Mtambo huo umekwenda sambamba na uwepo wa 'application' (App) ambayo pia imetengenezwa na vijana hao ikiwa na uwezo wa kunasa na kuhifadhi mawasiliano yote ya simu yaliyofanyika kutwa nzima.

App hii imeunganishwa kwenye simu za walimu shuleni hapo ambayo kazi yake ni kutoa taarifa kuhusu mawasiliano ya kutwa nzima yaliyofanyika na kunaswa na mtambo huo.

Kwa jinsi mtambo huo ulivyotengenezwa una uwezo wa kunasa endapo simu au ujumbe mfupi utaingia kwenye simu iliyo katika mazingira husika hata kama imefichwa sehemu gani, itatoa ishara kuonyesha kuna simu katika eneo hilo.

"Mwalimu hatopata ujumbe uliotumwa wala kusikiliza mazungumzo ya kwenye simu ila atapata taarifa kuwa kuna simu na kuanzia hapo ataweza kufuatilia hadi kubaini mahali ilipo na mhusika," anasema Reuben.

Haiishii hapo pia atakayejaribu kutumia intaneti kutafuta kitu chochote mtandaoni naye hatakuwa salama taarifa zake zitanaswa kama wale wanaopigiwa na kupokea ujumbe mfupi.

Tangu mtambo huo uanze kufanya kazi shuleni hapo tayari wanafunzi wanne wameshanaswa wakiwa wanatumia simu na hatua za kinidhamu zilichukuliwa dhidi yao.

## Mahusiano na wanafunzi wenzao

Wakati uongozi wa shule ukifurahia uwepo wa teknolojia hiyo kwa baadhi wa wanafunzi teknolojia hiyo imekuwa ni tatizo linalosababisha hadi kuwachukia wabunifu wa kifaa au mtambo huo.

Reuben anaeleza kuwa wamejikuta wakichukiwa na wanafunzi wenzao kwa kile wanachoamini wameiletea shule teknolojia inayowabana na kuwanyima uhuru wao.

Anasema hasira ya wanafunzi wenzao ilifika mbali kiasi cha kuuficha mtambo huo siku chache kabla ya kuja Dar kwa ajili ya kuonyesha ubunifu huo kwenye maonyesho ya wanasayansi wachanga.

"Lengo letu si kuwakomesha wenzetu tunataka sheria za shule zifuatwe wanafunzi tusome kwa bidii haipendezi mtu kuharibiwa maisha kwa kitu ambacho siku zote kitakuwepo utakutana nacho na

MWANANCHI.CO.TZ
JUMANNE, AGOSTI 14, 2018



Boris (kushoto) na Reuben wakionyesha kifaa walichokibuni ambacho kina uwezo wa kubaini matumizi ya simu mashuleni. Kifaa hicho kinaweza kutumiwa na walimu katika shule ambazo wanafunzi hawaruhusiwi kutumia simu. **Picha na Elizabeth Edward**

...ruhusiwi kutumia simu. **Picha na Elizabeth Edward**

utatumia hadi utachoka.

"Ila wenzetu wanahisi tofauti bahati nzuri mkuu wa shule siku zote anahakikisha tupo salama na kila siku jioni anamuagiza mlinzi aje kutuangalia bwenini kuhakikisha usalama wetu na taratibu wanafunzi wenzetu wanaanza kuelewa,"

Ndoto ya wanafunzi hao ambao wanasoma mchepuo wa sayansi wakichukua masomo ya Fikizia, Kemia na Hesabu ni kuongeza zaidi ujuzi wao kwenye fani ya ulinzi wa mtandao (cyber security).

"Hatufikirii kuishia hapa tunataka kuongeza ujuzi zaidi, akitokea mtu akatusaidia huko mbeleni itakuwa msaada mkubwa kwetu maana tunamaliza kidato cha sita muda si mrefu na tunatamani kusomea cyber security ili siku moja tubobee kwenye masuala hayo,"anasema Massesa

Mwalimu wa miradi katika shule ya Ilboru, Eudora Eliafye anasema wanafunzi hao walipomfuata kumuelezea kuhusu wazo lao aliwapokea kwa mikono miwili na kuwatia moyo.

Hilo lilitokana na wao pia kuchoshwa na kesi za matumizi ya simu kwa wanafunzi hivyo aliwaeleza vijana hao namna ya kufanya utafiti kabla ya kufikia kutengeneza mtambo huo.

"Tulipita kwenye shule saba mkoani Arusha tukijaribu kufanya utafiti wa matumizi ya simu kwa wanafunzi ndipo tukapata matokeo kwamba wengi wao wanazitumia kwa mambo yasiyofaa hivyo ikaonekana kweli ipo haja ya kuhakikisha matumizi ya simu shuleni yanakomeshwa.

"Ingawa tulifahamu kuwa vijana hawa wamefanya kazi kubwa lakini sikutegemea kama ingepokelewa vizuri namna hii hadi kufikia hatua ya kuibuka washindi kwenye kipengele cha teknolojia, najivunia wanafunzi hawa."

Miongoni mwa watu waliopata fursa ya kuuona mtambo huo ni Waziri wa Elimu Profesa Joyce Ndalichako. Naye alionyesha kuvutiwa na mradi huo na kuahidi kuufuatilia ili ikiwezekana uwekwe katika shue zote za Serikali.

Profesa Ndalichako anasema Serikali inaendelea kutafuta mwarobaini wa kuzuia matumizi ya simu za mikononi kwa wanafunzi wakiwa shuleni kwa kile alichodai kuwa zimekuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa matokeo mabaya hasa kwa shule za Serikali.

"Sheria haziruhusu mwanafunzi kuwa na simu lakini wengi wao wamekuwa wakitafuta namna ya kuwa nazo na kufanya mawasiliano ambayo kwa hakika hayana tija katika masomo yao na ndio sababu tunapata matokeo mabaya na mabweni kuungua moto, hii yote ni kwa sababu wanafunzi wanahangaika kuchaji simu," alisema Profesa Ndalichako.

Profesa Ndalichako pia anawatia moyo vijana na kuwasisitiza wasikate tamaa kwani ubunifu wao unahitajika hasa katika kipindi hiki ambacho nchi imejikita katika kujenga uchumi wa viwanda.

Anasema kwamba hakuna viwanda kama hakutakuwa na wanasayansi ambao watakuwa wanafanya kazi usiku na mchana kubuni teknolojia zitakazokuwa na tija kwa jamii inayowazunguka na Taifa kwa ujumla.

**Nipashe**

The story was published on August 3, 2018

***News summary***; the government has outlined the reason for special schools to drop during the YST exhibition that took place in Dar es Salaam.



8 **Nipashe** Ijumaa Agosti 3, 2018

**HABARI ZA KITAIFA**

# Sababu shule vipaji kushuka kitaaluma

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ametaja sababu ambazo zilikuwa zikichangia shule maalum za vipaji kushuka kitaaluma.

Moja ya sababu hizo alisema ni kukosekana kwa usimamizi mzuri wa shule hizo na usimamizi mzuri wa uchujwaji wa wanafunzi wanaojiunga katika shule hizo.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha inasimamiwa vizuri kuzilinda pamoja na kuweka utaratibu maalum, ili ziendelee kuwa na heshima yake.

"Shule za sekondari za vipaji zilikosa usimamizi na pia utaratibu wa kuchuja wanafunzi wanaokwenda kwenye shule hizo haukuwa unafanyika vizuri, na ndio maana ukachangia shule hizi kushuka kitaaluma, tunatakawanafunzi wenye uwezo mkubwa wapate elimu kulingana na uwezo wao," alisema Prof. Ndalichako na kuongeza:

"Tayari tumekwishaweka utaratibu kuhakikisha zile shule zetu za vipaji ikiwamo Ilboru, Kilakala, Mzumbe na nyinginezo za vipaji kuwa na heshima na hadhi yake, tumegundua kwamba baadhi ya wanafunzi ambao wamekuwa wakienda katika shule hizo hawana zile sifa ambazo shule zinahitaji, kwa hiyo tumejipanga kulinda heshima yake kwa kuimarisha usimamizi na utaratibu wa mchujo wa wanafunzi."

Alisema serikali imefurahia matokeo ya kidato cha sita shule za serikali kuongoza na kwamba inajipanga kuziboresha ili kuhakikisha na matokeo ya kidato cha nne nayo yanakuwa mazuri.

Prof. Ndalichako alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akifunga maonyesho ya nane ya wanasayansi chipukizi yaliyoandaliwa na Shirika la Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST).

Profesa Ndalichako pia aliiomba Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTEC), kusimamia vipaji vya ubunifu wa kisayansi kwa wanafunzi shuleni kuanzia ngazi ya awali hadi juu.

Alisema COSTEC ina umuhimu mkubwa wa kuangalia vipaji hivyo kwa kuangalia namna gani wanaweza kuvitumia katika kuboresha utafiti wao.

"Kuna mradi nimeuona unatumia nywele kutengeneza mbolea, hivyo ubunifu huo unabidi kuendelezwa ili kuwawezesha vijana wetu kufanya vitu vikubwa kwa maendeleo ya taifa.

"Sayansi ina umuhimu sana kwa sababu mambo tuliyoyaiga yalianza kubuniwa na mtu, sasa kupitia vijana hao Tanzania tutapata vijana wataisababishia dunia kutambua kitu kilichogundulika nchini," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa YST, Dk. Gozbert Kamugisha, alisema maonyesho hayo yamewashirikisha wanafunzi 200 na walimu 100 kutoka mikoa yote nchini.

Alisema tangu kuanzishwa kwa maonyesho hayo mwaka 2012, jumla ya wanafunzi 5000 walishirikiana na walimu 1,000 kupatiwa mafunzo ya jinsi ya kufanya utafiti.

**Mtanzania**

The story was published on August 4, 2018

**News summary**; the Minister for education, science and technology  amazedby how hairs canbe changed intomanure



UBUNIFU

## Nywele zinazotengeneza mbolea zamshangaza Prof. Ndalichako

Na TUNU NASSORO

WAZIRI Wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, ameshangazwa na teknolojia ya kutengeneza mbolea kwa kutumia nywele huku akiiagiza Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTEC), kuvisimamia vipaji vya ubunifu wa kisayansi kwa wanasayansi chipukizi.

Akizungumza katika sherehe za utoaji zawadi kwa washindi, katika maonesho ya nane ya Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi Nchini(YST) zilizofanyika Dar es Salaam, Profesa Ndalichako alisema vimekuwapo vipaji kwa wanafunzi mashuleni lakini vinashindwa kuendelezwa.

Alisema kazi ya COSTEC ni kuangalia vipaji hivyo na kuangalia jinsi wanavyoweza kuboresha tafiti zao na kutatua changamoto zinazoikabili jamii.

"Kuna mradi nimeuona unatumia nywele kutengeneza mbolea, ubunifu huo unabidi kuendelezwa ili kuwawezesha vijana wetu kufanya vitu vikubwa kwa Maendeleo ya taifa,"alisema Profesa Ndalichako.

Alisema vitu vingi vilivyotengenezwa kwa teknolojia, vilibuniwa na watu katika mataifa yao na kuendelezwa hivyo na Tanzania ikisimamia vipaji vya watu wake, itaweza kuibua ubunifu ambao utaiendeleza nchi kufikia ndoto ya uchumi wa viwanda.

"Sayansi ina umuhimu sana kwa sababu mambo tuliyoyaiga yalianza kubuniwa na mtu, sasa kupitia vijana hawa wataisababishia dunia kutambua kitu kilichotengenezwa nchini mwetu," alisema Profesa Ndalichako.

Katika hatua nyingine, Profesa Joyce alisema Serikali inaweka utaratibu wa kuziwezesha shule za vipaji maalumu ili zirudishe heshima kwa kuwa zilipoteza mwelekeo kwa kupelekewa wanafunzi wasiokidhi vigezo.

"Tatizo la shule hizo kuonekana kufanya vibaya ilikuwa ni wanafunzi kutochujwa vizuri katika mitihani yao, sasa tutaziwezesha ili kuongeza chachu katika ufaulu," alisema.

**Tanzania Daima newspaper**

**News summary**; the Minister for education, science and technology has been impressed by science creativity of secondary students



# Ubunifu wa wanafunzi ulivyomgusa Waziri Ndalichako

Uk. 12&13

*Mwanafunzi wa shule ya Sekondari ya mtakatifu Joseph Kolping, Fransisco Solomon akionesha roboti waliyoitengeneza kwa ajili ya kulinda barabarani.*

NA MAGRETH KABYEMELA

UTAFITI unajumuisha kazi ya ubunifu iliyofanywa kwa misingi ya utaratibu ili kuongeza maarifa ya elimu, ikiwa ni pamoja na ujuzi wa wanadamu, utamaduni na jamii na matumizi ya ujuzi katika kuunda vitu vipya.

Pia, tafiti zimekuwa zinatumika kuanzisha au kuthibitisha ukweli, kuthibitisha matokeo ya kazi ya awali, kutatua matatizo mapya au yaliyopo, msaada wa nadharia, au kuendeleza nadharia mpya.

Kwa mantiki hiyo, mradi wa utafiti unaweza pia kuwa upanuzi wa kazi ya zamani katika shamba.

Miradi ya utafiti inaweza kutumika kuendeleza ujuzi zaidi juu ya mada au kwa mfano wa mradi wa utafiti wa shule, inaweza kutumika kwa kuendelea utafiti wa mwanafunzi wa uwezo wa kuwaandaa kwa ajira au ripoti za baadaye.

Katika kuthibitisha uhalali wa vyombo, taratibu au majaribio, utafiti unaweza kuiga vipengele vya miradi ya awali au mradi kwa ujumla.

Madhumuni ya msingi ya utafiti wa msingi (kinyume na utafiti uliotumika), ni nyaraka, ugunduzi, ufafanuzi, au utafiti na maendeleo (R & D) ya njia na mifumo ya maendeleo ya ujuzi wa binadamu.

Hata hivyo, mbinu za utafiti hutegemea epistemologies, ambazo hutofautiana sana ndani na kati ya wanadamu na sayansi.

Ukija katika aina za utafiti; zipo za kisayansi, wanadamu, kisanii, kiuchumi, kijamii, biashara, masoko, utafiti wa wataalamu, maisha pamoja na teknolojia.

Kwa kutambua umuhimu wa tafiti katika kukuza maarifa na ujuzi wa wanafunzi na manufaa yake kwa taifa, Shirika la Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST) limekuwa likiratibu shindano la kazi za kitafiti kwa wanafunzi wa sekondari zaidi ya 200 kila mwaka.

Safari hii, maonyesho ya kazi hizo za wanafunzi yalifanyika katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC), jijini Dar se Salaam

mafunzo kutoka kwa washauri wa sayansi wa YST kuhusu namna ya kutengeneza kazi zao za kisayansi.

Katika kuhimiza wanafunzi kuyapenda zaidi masomo ya Sayansi, Kamugisha anatoa wito kwa wazazi/ walezi, walimu na jamii, kila mmoja kwa nafasi yake awekeze nguvu kazi kwa kutenga muda wake kuhamasisha watoto kupenda masomo ya Sayansi.

Kwamba, jambo hilo ni muhimu kwa ajili ya kuipatia nchi wataalamu na wagunduzi watakaoipeleka katika Tanzania ya uchumi wa kati ifikapo 2025 kupitia uwekezaji wa nguvu katika sekta ya viwanda.

Kamugisha ambaye taasisi yake imefanya maonyesho yake kwa ya nane, anasema ametiwa moyo na miradi mbalimbali ya kisayansi iliyogunduliwa na wanafunzi zaidi ya 200 kutoka shule binafsi na serikali kutoka mikoa yote ya Tanzania.

Anasema, shirika hilo lililoanzishwa mwaka 2011 kwa lengo la kuhamasisha wanafunzi wa shule za sekondari zote nchini kusoma masomo ya sayansi na kuyafanya kwa vitendo zaidi, matunda yake yameanza kuonekana.

"Tuliamua kuanzisha shirika baada ya kufanya utafiti na kugundua kuna msukumo mdogo wa wanafunzi kupenda masomo ya sayansi.

"Tuliona, tukianzisha shirika ili kufumua mifumo ya fikra hasi kwa wototo ambayo ilikuwa imeota mizizi kwa miaka hiyo kuwa masomo ya sayansi ni magumu na hayawezekani alisema Kamgisha na kuongeza:

"Tulianzisha mpango wa kuwafundisha walimu kwa maana ya kuwapa ujuzi wa ni namna gani amfundisha mtoto na afikie kufanya utafiti wa kisayansi kwa maana ya ugunduzi katika Nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

"Tulilenga ugunduzi huu ulenge jamii mfano katika kilimo na ufugaji ambapo kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanao soma masomo ya sayansi sambamba na ufaulu ambao wanafanya ugunduzi wa

tabia za kijamii (social behavior), mfumo wa viumbe hai vinavyotegemeana (biological ecological).

Mengine ni physics (phyzikia) kemia na hesabu zote hizi katika makundi yake washindi walijinyakulia zawadi za pesa tasilimu na wachache kati yao washindi wa jumla wanapewa udhamini wa kulipiwa elimu ya vyuo vikuu katika masomo ya sayansi.

Akizungumza baada ya ufunguzi rasmi wa maonyesho hayo, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako anasema maonyesho hayo ya tafiti za kazi za kisayansi yataisaidia serikali kuboresha ufaulu kwa wanafunzi.

Kwamba, licha ya kuwepo marufuku ya matumizi ya simu shuleni, wamekuwa wakaidi wakizitumia kiujanja ujanja jambo ambalo wenzao wamegundua teknolojia ya kuzibaini simu zilizofichwa kwa kutumia utafiti wa kiyansi hata kama zimefichwa ardhini.

"Tunapata tabu sana na wanafunzi tunawakataza kutumia simu za mkononi lakini wanaunganisha waya kwa njia za ajabu ambazo wakati mwingine zinaweza kusababisha majanga ya moto shuleni.

Ni simu hizo za mikononi ambazo wakati mwingine ninasababisha shule za Serikali kutofanya vizuri katika mitihani yao kwa sababu muda mwingi wanafunzi wanautumia katika simu.

"Lakini sasa, nafurahi sana wanafunzi wamekuja na teknolojia ya kuzifichua simu zilizofishwa chini ya mti na ardhini jambo ambalo nitaliunga mkono ili litumike katika shule zote za Sekondari.

"Kadhalika, nimependa mradi (project) inayotoa elimu juu ya saratani ya mlango wa kizazi namna ya kujikinga na saratani hiyo kwa kuepuka visababishi.

"Kwa kweli wanafunzi mmetisha, nawapongeza sana kwa kumpa moyo Rais Magufuli katika dhamira yake ya kuendeleza sayansi na teknolojia.

"Wafadhili wote mliofanikisha hili nawapongeza kwa uzalendo wa



*Waziri Wa Elimu Sayansi na Teknolojia , Profesa Joyce Ndalichako akitoa zawadi kwa Wanafunzi wa Msalato sekondari ambao, washindi wa jumla wa Maonesho ya Wanasayansi chipukizi 2018. Ni wilhelmina na Farida*



*Mwanafunzi wa shule ya Sekondari ya Vingunguti, Neema Julius akieleza namna mazingaombwe yana uhalisia wa sayansi tofauti na wanajamii wanavyofikiri.*

kuviendeleza.

Katika maonyesho hayo wanafunzi waliochukua nafasi ya kwanza kabisa katika vinyang'anyiro vyote ni kutoka shule ya Sekondari ya Msalato chini ya mradi wa kuchenjua chumvi katika mmea wa mbigiri ambao kwa asili unamiiba.

"Mmea huo una chumvi na madini, lakini wanyama hawawezi kuula kwa sababu ya miiba.

"Hivyo wanafunzi hao chini ya usimamizi wa mwalimu wao Sales Ibrahimu, mkuu wa idara ya Kemia, waliamua kuukausha mmea huo na kuuingiza katika maabara kwa utafiti wa kisayansi ambao wamebaini madini na chumvi ambayo inapatikana katka mbigiri vikiongezwa katika chakula cha wanyama vinaongeza hamu ya kula, hivyo kuwaongezea wanyama virutubisho na madini.

***Mwandishi anapatikana kwa namba 0767697690***



***Mwanzilishi mwenza wa YST, Dr. Gosbert Kamugisha akipata maelezo kuhusu matumizi ya umeme wa upepo, sauti, na mtetemo kutoka kwa mwanafunzi wa Same Sekondari, Samwel Osebius.***

daimanews@yahoo.com

**BLOGS**

**JIJILETU BLOG**

The story was published on August 3, 2018 after the exhibition

Link of the story; Jijiletublog.blogspot.com/2018/08/ndalichako-akabidhi-tuzo-kwa-washindi.html

***News summary***; Minister for education, science and technology Prof Joyce Ndalichako present a trophy to winners of the YST exhibition 2018

**Friday, August 3, 2018**

**NDALICHAKO AKABIDHI TUZO KWA WASHINDI WA JUMLA WA MAONESHO YA YST**



WaziriWa Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako akizungumza wakati wa kufunga Maonesho ya Wanasayansi Chipukizi yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.



Balozi wa Uingereza Sarah Cooke akizungumza wakati wa Maonesho ya Wanasayansi Chipukizi nchini



WaziriWa Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako akitoa zawadi kwa Wanafunzi wa Msalato sekondari ambao ndio washindi wa jumla wa Maonesho ya Wanasayansi chipukizi 2018 ambao ni wilhelmina and Farida



Waziriwa Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako akiwa katika picha ya pamoja na washindi katika Maonesho ya Wanasayansi Chipukizi 2018.



Baadhi ya Wanafuzi walioshiriki katika Maonesho hayo wakifatilia utoaji wa tuzo hiz

**MICHUZI Blog**
The story was published on August 7, 2018

https://issamichuzi.blogspot.com/2018/07/wanafunzi-200-shule-mbalimbali-za.html

**FACEBOOK LIVE COVERAGE**

The Award Ceremony was aired live through YST Facebook and it had made 15,988 Views on a the social media platform/

PREPARED BY:

CRISPIN GERALD

PR CONSULTANT FOR YST

Mikocheni Light Industrial Area

P.O Box 31042

Mob: +255 713 288246

Office Tel; +255 788648241

Email: crispinsamson1@gmail.com

crispin_gerald@ymail.com

Twitter: @crispintz

Facebook: Crispin Samson.